

19- Idhwhaar Na Idghaam Katika Laam

Idhwhaar na Idghaam katika Laam :

ل (Laam) ya المعرفة (al-ma'rifah- kibainishi) inapokuwa mbele ya herufi za hijaaayah hugawika katika hali mbili; Herufi za الشَّمْسِيَّة (ash-shamsiyah - jua) na za الْقَمَرِيَّة (al-qamariyah - mwezi). ل hiyo hutamkwa ima kwa idhwhaar au kwa idghaam.

Idhwhaar katika Laam :

ل (Laam) ya kibainishi yenye kuingia katika jina hudhihirishwa inapokuwa herufi inayoifuatia ni katika herufi za qamariyyah; ambazo zimekusanyika katika ibara:

أَبِغْ حَجَّكَ وَخَفْ عَقِيمَهُ

Herufi za qamariyyah zimeitwa hivyo kwa kuwa huwajibika kudhihirisha ل iliyoko kabla ya hizo herufi kama inavyodhihirishwa katika neno la الْقَمَر (al-Qamar - mwezi) na alama yake ni kuweko sukuwn.

Idghaam katika Laam :

ل (Laam) ya kibainishi iliyo saakin huingizwa kwenye herufi inayoifuatia ikiwa herufi hiyo ni katika herufi za shamsiyyah (jua) ambazo ni herufi zote zisizokuwa herufi za qamariyyah (mwezi); nazo zimekusanyika katika kila mwanzo wa neno kwenye ibara:

طَبَّ ثُمَّ صِلْ رَحِمًا تَفُزْ صَفْ ذَا نَعَمْ دَعْ سُوءَ ظَنِّ زُرْ شَرِيفًا لِلْكَرَمِ

Herufi za shamsiyyah: Zimeitwa hivyo kwa kuwa huwajibika kuingiza ndani yake ل iliyoko kabla ya hizo herufi kama inavyoingizwa katika neno الشَّمْس (ash-shams - jua) na alama yake ni kutokuweko sukuwn na kuweko shaddah katika herufi inayofuatia.

Herufi za shamsiyah Idghaam			Herufi za qamariyah Idhwhaar		
Matamshi	Neno	Herufi	Matamshi	Neno	Herufi
at-twufaan	الطُّوفَانَ	ط	al-Aakhirah	الْآخِرَةُ	أ ء
ath-thamaaraat	الْتَّمَرَاتِ	ث	al-ba'th	الْبَعْثِ	ب
as-Swalaah	الصَّلَاةَ	ص	al-ghayth	الْغَيْثِ	غ
ar-Ra'd	الرَّعْدُ	ر	al-haqq	الْحَقُّ	ح
At-Ttawwaab	التَّوَابِ	ت	al-Jannah	الْجَنَّةَ	ج
adhw-dhwalaalah	الضَّلَالَةَ	ض	al-Kawthar	الْكَوْثَرَ	ك
adh-dhaakiriyn	الذَّاكِرِينَ	ذ	al-wuhuwsh	الْوُحُوشُ	و
an-nakhl	النَّخْلِ	ن	al-khayraat	الْخَيْرَاتِ	خ
ad-duniyaa	الدُّنْيَا	د	al-fiyl	الْفَيْلِ	ف
as-samaaaa	السَّمَاءِ	س	al-'abd	الْعَبْدُ	ع
adhw-dhwulumaat	الظُّلْمَتِ	ظ	al-Qiyaamah	الْقِيَامَةِ	ق
az-zaytuun	الزَّيْتُونِ	ز	al-yawm	الْيَوْمِ	ي
ash-sharr	الشَّرِّ	ش	al-Muddath-thir	الْمُدَّتِيرِ	م
al-layl	الَّيْلِ	ل	al-Hudaa	الْهُدَى	ه